Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# MKUTANO WA KUMI NA SITA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA TATU - TAREHE 12 JULAI 2004

Dua Kusomwa na

Kikao Kuanza Saa Tatu Asubuhi

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

### WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Chai Tanzania kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2003, *[The Annual Report and Accounts of the Tea Board of Tanzania for the Year ended 30$^{th}$ June, 2003].*

### WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

### MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

## II. MASWALI

### OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):

**217. MHESHIMIWA SHIBILITI (MISUNGWI):** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa:- Kwa kuwa Wilaya ya Misungwi ni miongoni mwa Wilaya zisizokuwa na huduma muhimu za Hospitali ya Wilaya; na kwa kuwa kumekuwepo na juhudi za kupanua Kituo cha Afya Misungwi kwa ujenzi wa chumba cha X- ray, ujenzi wa wodi ya wagonjwa kwa nguvu za wananchi:-

(a) Je, kituo cha afya – Misungwi kinachotumika kama hospitali kitapewa lini hadhi ya kuwa hospitali ya Wilaya;

(b) Je, Serikali imejiandaaje kusaidia nguvu za wananchi ikiwa ni pamoja na kuongeza waganga;

(c) Je, ni zahanati zipi mpya zimefunguliwa Wilayani humo kupunguza msongamano wa wagonjwa kutokana na ongezeko la watu.

**218. MHESHIMIWA LAIZER (LONGIDO):** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa):- Kwa kuwa katika hotuba ya bajeti (ya mwaka wa Fedha 2003/2004) ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), alieleza kwamba Ofisi za Wabunge zitajengwa kwenye Makao Makuu ya Wilaya; na kwa kuwa majimbo mengine yako mbali na Makao Makuu ya Wilaya, na baadhi ya wananchi watashindwa kutembea umbali huo kuonana na Wabunge wao:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba ni gharama kubwa kwenda kwenye ofisi iliyoko mbali na jimbo husika;

(b) Je, Serikali haioni kwamba wananchi watamlaumu Mbunge wao kwa kuona kwamba amewatoroka.

**OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):**

**219. MHESHIMIWA RAMADHANI HASHIM KHALIFAN (BAGAMOYO):** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora):- Kwa kuwa tatizo la rushwa limekuwa kero kubwa, na limekuwa na dosari kubwa katika nchi yetu mbele ya Watanzania na hata Jumuiya za Kimataifa; na kwa kuwa juhudi za kupambana na tatizo hilo zimeanza tangu enzi za ukoloni mwaka 1930 ilipowekwa mikakati thabiti ya kulikabili, na baadaye mwaka 1958 kutungwa sheria ya '*Prevention of Corruption Ordinance' (Cap.400),* na mnamo mwaka 1971 Serikali ilitunga sheria Na.16 kulidhibiti tatizo hilo na baada ya miaka mitatu kilianzishwa kikosi maalum cha kuzuia rushwa chini ya sheria Na.2 ya mwaka 1974 na majukumu yake yaliainishwa katika kifungu cha 2A (3) (a), (b), (c) na baadaye jina la kikosi hicho likabadilishwa mwaka 1991 kwa tangazo la Serikali Na. 27 na kuwa Tume ya Kupambana na Rushwa yenye Mkurugenzi Mkuu na Wakurugenzi wengine wanne (4):-

(a) Je, Serikali haioni kwamba wakati sasa umefika wa kuiangalia upya sheria hiyo pamoja na vyombo vya utekelezaji vilivyoundwa chini yake ili kukomesha kabisa rushwa nchini;

(b) Je, Serikali itakubali kuwa utaratibu wa kuwashitaki watoaji/na wapokeaji rushwa unaifanya vita hiyo iwe ngumu sana, na kwamba utaratibu huo unaishamirisha rushwa badala ya kuiondoa;

(c) Kwa kuwa ni dhahiri kabisa, na tunafahamu kwamba mlaji rushwa hutumia umahiri kutengeneza mazingira yatakayomwezesha hata asiyependa kutoa rushwa alazimike kufanya hivyo, au vinginevyo “ale jeuri yake” na mahali pengine hata apoteze maisha; Je, kwa nini Serikali isianze sasa kumshughulikia anayepokea rushwa na huku ikimtumia mtoaji rushwa kama shahidi wake.

**WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA:**

**220. MHESHIMIWA LUPATU (KOROGWE MAGHARIBI):**
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula:- Kwa kuwa umezuka mtindo wa baadhi ya waajiri hasa wa kampuni binafsi wa kutowalipa mishahara wafanyakazi wao, na kulimbikiza madeni makubwa ya mishahara na kuwaletea adha kubwa wafanyakazi hao, kwa mfano Kampuni za Chai za Dindira na Ambangulu; na baadhi ya mashamba ya Mkonge katika Wilaya ya Korogwe:-

(a) Je, Serikali inatoa ushauri gani kwa wafanyakazi hao wanaonyimwa haki zao;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti/kuzuia dhuluma ya namna hiyo;

(c) Kwa kuwa Serikali iliahidi Bungeni kuwa wafanyakazi wa Mashamba ya Chai ya Dindira na Ambangulu watalipwa malimbikizo ya mishahara yao ifikapo tarehe 30 Juni, 2002; Je mpaka sasa wameshalipwa kiasi gani.

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

**221. MHESHIMIWA RWILOMBA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kwa kuwa umeme ni muhimu sana katika maendeleo ya Jamii; na kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo wa Dhahabu wanahitaji umeme na elimu ambayo pia inahitaji umeme:-

(a) Je, Serikali itapeleka lini umeme katika vijiji vya Nyakagwe, Bukoli, Nyamalimbe, Rwangasa, Nyarugusu, Kaseme, Katoro na Butundwe ili wachimbaji wadogo wadogo waweze kuzalisha dhahabu;

(b) Je, Serikali itapeleka lini umeme katika shule zilizojengwa katika maeneo hayo ili wanafunzi wajifunze teknolojia mpya ya kompyuta;

(c) Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kupeleka umeme Bukombe; Je, kwa nini isipitishe umeme huo Bukoli, Nyarugusu, Rwangasa, Katoro hadi Bukombe njia ambayo ni fupi kwenda Bukombe.

**WIZARA YA USHIRIKA NA MASOKO:**

**222. MHESHIMIWA SINGO (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko:- Kwa kuwa miundo mbinu ya Kilimo na Masoko Wilayani Same Mkoani Kilimanjaro imedhihirika kuwa ni duni na hivyo kukwamisha juhudi za Serikali za kupambana na umasikini; na kwa kuwa ili kukabili kasoro hizo Serikali ilianzisha Taasisi ya Mpango wa Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (Agricultural Marketing Systems Development Programme) katika Ofisi ya Waziri Mkuu:-

(a) Je, ni lini Taasisi hiyo itaanzisha huduma zake katika Wilaya ya Same na ni katika maeneo gani ya Kilimo na Masoko;

(b) Je, Wakulima, Wafugaji na Wafanyabiashara watafaidikaje na taasisi hiyo;

(c) Ni kwa namna gani kila mdau ajiandae kupokea huduma ya taasisi hiyo.

**WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI:**

**223. MHESHIMIWA MULYAMBATTE (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni:- Kwa kuwa Maktaba ya Mkoa wa Shinyanga ni ndogo sana na haina vitabu vya kutosha kulingana na watumiaji wa Maktaba hiyo:-

(a) Je, ni lini Serikali itaiongeza Maktaba hiyo ili iweze kukidhi mahitaji ya watumiaji;

(b) Je, ni lini Serikali itaongeza vifaa na vitabu katika maktaba hiyo, na kueleza mapungufu mengine muhimu kwenye maktaba hiyo.

**224. MHESHIMIWA SHEKIFU (LUSHOTO):** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni:- Kwa kuwa mnamo mwaka 2001 Bweni la Shule ya Sekondari ya Magamba iliyoko Wilayani Lushoto liliungua kwa moto na kuteketea kabisa; na kwa kuwa kutokana na janga hilo Shule imekumbwa na tatizo kubwa la kupokea idadi ya wanafunzi takriban 90 kila mwaka; na kwa kuwa hadi leo bweni hilo halijajengwa jambo ambalo linaathiri sana upokeaji wa wanafunzi kwa maana ya kupungua kwa idadi ya wanafunzi wanaopokelewa shuleni hapo kwa mwaka:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kulitatua tatizo hilo;

(b) Kwa kuwa majengo ya shule hiyo yalijengwa kwenye miaka ya 1960 na kwamba sasa yamechakaa sana kiasi kwamba yanahitaji ukarabati mkubwa kwa sababu hayakufanyiwa ukarabati mdogo mdogo kwa kipindi kirefu; Je, Serikali itachukua hatua gani za dhati za kuyafanyia ukarabati majengo ya shule hiyo.

**WIZARA YA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**

**225. MHESHIMIWA MUSALIKA (NYANG'HWALE):** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo:- Kwa kuwa wapo Watanzania walioshiriki kupigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia chini ya

Jeshi la Mwingereza; na kwa kuwa maveterani hao wa vita kwa muda mrefu sasa wameahidiwa kupewa asante (honoraria) kutoka Uingereza pesa ambayo inasemekana ililetwa nchini lakini watu wachache wajanja wakaila:-

(a) Je, Serikali ina maelezo gani ya kina juu ya suala hilo na kwamba itakuwa tayari kutoa maelezo hayo kwa Wakuu wa Wilaya na kuwaeleza wawafikishie walengwa badala ya hali ilivyo sasa ambapo Waheshimiwa Wabunge wanaulizwa na wapiga kura wao juu ya fedha hizo na wengi wanakuwa na kigugumizi kwa kutokuwa na jibu sahihi la kuwapa;

(b) Kama fedha hizo zimetumiwa au zimepotea, Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutenga fungu la fedha maalum kwa ajili ya kuwalipa hao wazee wahusika ambao mchango wao ni muhimu sana katika historia ya nchi yetu na wakati huo huo Serikali itafute njia ya kurudisha fedha hizo toka mikononi mwa watu waliozipokea.

## III. HOJA ZA SERIKALI

### WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

## IV. SAA 6.00 MCHANA:

### HOTUBA YA RAIS WA NAMIBIA MHESHIMIWA SAM NUJOMA

**DODOMA** — **K.M.M**
**12 JULAI, 2004** — **KATIBU WA BUNGE**